

Limejengwa katika Wagalatia 4:21-31.

A Agano pamoja na Adamu na Hawa.

- ❖ Kabla ya dhambi (Mwanzo 2), agano lilijumuisha angalao vifungu vifuatavyo kwa ajili ya mwanadamu:
 - Itunze Sabato (fg. 3).
 - Tunza uumbaji (fg. 15).
 - Usile tunda la ujuzi wa mema na mabaya (fg. 17).
- ❖ Ilikuwa wazi kabisa: Tii nawe utaishi! Ni dhahiri, Adamu na hawa wengeweza kutimiza agano hilo, walikuwa viumbe wakamilifu.
- ❖ Tangu walipoasi, Mungu alitambulisha agano jipya la neema lenye msingi katika ahadi ya Mwokozi (Mwanzo 3:15)

B AGANO PAMOJA NA IBRAHIMU.

- ❖ Mungu alipomuita Abram, aliahidi kumfanya “taifa kubwa”, Hivyo, Mungu akafanya agano imara na Abram kwa kutembea kati ya miili iliyotenganishwa ya wanyama walitolewa kafara (Mwanzo 15:9-21).
- ❖ Kwa kufanya hivyo, Mungu akahakikisha agano Lake kwa uhai wake mwenyewe. Mwishoni anatoa uhai wake Kalwari kutimiza ahadi.

C Sara na Hajiri.

- ❖ Kosa la kwanza la Abram lilikuwa kuondoka nchi ya ahadi na kwenda Misri. Baadhi ya watumwa ambao Farao alimpa Sara waliungana na msafara wa Abram. Hajiri alikuwa mmoja wao..
- ❖ Sarai alikuwa tasa, hivyo baada yakusubiri kwa miaka kumi, alifikiri anaweza kupata mwana kwa kumtumia mtumwa wake kama “mama mbadala” kumzalia mtoto.
- ❖ Kwa hiyo, Ishmaeli ni matokeo ya juhudi ya kibinadamu (“kwa mwili”) wakati Isaka alikuwa mwana wa Sara na matokeo ya imani (“kwa ahadi”, Wagalatia 4:23).

D Hajiri na Sinai.

- ❖ watu hawakuweza kutunza agano hilo, kwani walijaribu kulitunza kwa njia zao wenyewe na kuishusha imani kwenye nafasi ya pili (Waebrania 4:2; Kutoka 19:8).
- ❖ ***Kwa njia hiyo hiyo Ibrahimu na Sara walijaribu kumsaidia Mungu kutimiza ahadi Zake, tWaisraeli walitafuta kugeuza agano la Mungu la neema kuwa agano la matendo. Hajiri ni mfano wa Sinai ambapo hufunua majaribio ya kibinadamu kwa wokovu kupitia matendo.***

E Ishmaeli na Isaka.

- ❖ Wokovu kwa matendo na wokovu kwa Imani havishikamani. Tunahitaji “kufukuza” moja ya njia hizo mbili za wokovu (Wagalatia 4:30).
- ❖ Ishmaeli alimuudhi Isaka kuchukua urithi wake. “Wana wa mwili” pia huwaudhi “wana wa Roho.”

“na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia.” (Mwanzo 26:4)

ABRAMU

Hajiri alikuwa zawadi kutoka kwa Farao, mtumwa. Sara alikuwa mke halali wa Abramumu.

HAJIRI

SARA

Ishmaeli alikuwa mgomvi. Isaka alikuwa mpenda amani.

ISHMAELI

ISAKA

Baadhi ya watu huitazama Sinai na kujaribu kuokolewa kwa matendo yao. Sisi tunamtazama Kristo na tunaokolewa kwa imani.

**MLIMA
SINAI**

AHADI

Baadhi ya watu huamini kile wanachoweza kufanya katika maisha haya. Sisi tunaamini kilie ambacho Mungu amekwishatufanyia.

**YERUSALEMI
YA KIDUNIA**

**YERUSALEMI
MPYA**

Baadhi ya watu ni watumwa wa matendo yake. Sisi tuko huru katika Yesu Kristo Mwokozi wetu.

WATUMWA

HURU